

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam**  
**8 Novemba 2008**

**Waliohudhuria**

Bashiri Rashidi  
Beda John Mkusu  
Canon Malicia  
Elaine Baker  
Filbert Mbecha  
Frank Peter Rwechungura  
George Kabogo  
Hamadi Hatibu Bwaja  
Idrisa Kessi Zongo  
John Hamock  
John West  
Juma Ali Salehe Jongo  
Juma Hassan Chibaya  
Kibwana Mohammad Msiga  
Mohamed S. Mwenguo  
Mohammed Samwely  
Mwamaisha Khamisi  
Paulo Atibu Hatibu  
Shamte J Kigoma  
Yusuf Mboga

**Wanachama wapya**

Wanachama wapya walijitambulisha. Kuna wanafunzi wa shule wawili, Mwanaisha ambaye ni mpanda baisikeli mlemauvu na John West anayetoka Chigaco Merekani na ni mwanachama wa chama cha baisikeli “critical mass” pale. Pia amesoma mipango ya jiji chuo kikuu. Atakuwepo Tanzania mwaka moja lakini Dar es Salaam mwezi mmoja tu halafu Tanga. Alisema Chigaco walibadalisha reli za zamani ziwe njia za banskeli.

**Msafara wa Baiskeli**

Elaine aliandika repoti ya kifedha na alisambaza kwa wanachama. Pia aliandika repoti kwenye website na aliweka picha kule. Anahitaji kusanya risiti kutoka Mejah ili kutayarisha repoti kwa ajili ya ubalozi wa Ireland.

### **Mradi wa Wamba**

Elaine aliwasiliana na mwalimu mkuu shule ya Mbondole, Msongole. Alipendekeza tufanye mafunzo kwa masaa matatu kila siku kwa siku nne badala ya siku mbili nzima. Ana wanafunzi 60 students wapanda baiskeli ambao watashiriki. Alipendekeza tufanye kati ya tarehe 17 - 26 Novemba. Bashiri, Filbert, Frank Peter, Hamadi, Kibwana, Mohammed Samwel na Paulo walisema wako tayari kufundisha. Ally Athman ambaye hayupo anajua njia kwenda kwenye shule. Wanachama pia walipendekeza Hussein Hamza na Edgar. Kwenye mpango wetu tuna nafasi ya walimu wawili kwa kila wanafunzi 20 basi tunaweza kuwagawa kwenye kundi tatu na kuwa na walimu sita. Tuliamua kuchangua walimu kwenye mkutano ujao. Tuliamau waalimu wataendesha baiskeli mpaka Msongole na kulala pale baadala ya kusafiri kila siku. Tuwe na badjeti ya chakula kwa waalimu, chai na andazi kila siku kwa wanafunzi na zawadi kwa wanafunzi.

### **Kongamano**

Elaine anajaribu kupata taarifa ya idara gani kwenye serekali ya jiji inashughulika na usafiri ili tuongee nao kuhusu kongamano. Pia alitumia email kwa contacts mbali mbali kupata ushauri. John alisema anamfahamu mtu wa Canada anayefanya kazi serekali ya jiji na atawasiliana naye. Pia Elaine atajaribu kuwapigia simu lakini wiki jana simu hazikufanya kazi. Pia Elaine aliwasiliana na diwani Lupilya ambaye alisema atajaribu kupata appointment na meya wa jiji.

### **Mkutano wa ubora wa hewa, Kenya**

Elaine alileta nakala ya makubaliano yameyotoka mkutano wa ubora wa hewa, Nairobi ambao Mejah alihudhuria. Ndani yake kuna ahadi kuhusu kuhamasisha usafiri wa siyo ya moto.

Pia kwenye maada moja walikuwa na picha tatu ya barabara moja – picha moja in magari binafsi 50, nyingine ina mabasi mawili na watu 50 ndani na nyingine ina wapanda baiskeli 50. Tutapenda kufanya photo kama hiyo hapa Dar es Salaam ili kuonyesha shida ya msongamano inasababisha na nini.

### **Redio**

Mejah alizungumza kwenye redio jana ijumaa kuhusu masuala ya baiskeli kwenye kipindi cha mazingira radio one. Walimwomba arudi tena baada ya wiki mbili.

### **Mashindano ya wimbo**

Shamte alikuwa na wazo la mashindano ya wimbo tualike watu kuandika na kuimba wimbo kuhusu baisikeli Dar es Salaam na tunachagua wimbo bora na tunapata wadhamini kurekodi.

### **Mambo ya hela**

Juma alitumia Tsh 5,000 kwa betri ya simu anayetumia kwa mawasiliano ya UWABA. Wanachama walisema kama kuna matumizi zaidi ya Tsh 3,000 bora aongee na wanachama kwenye mkutano kwanza kabla ya kutumia. Hela ya guta haikuletwa kwenye mkutano. Wanachama walipendekeza Ally Saidi Mwishehe aje kwenye mikutano kutoa repoti kuhusu guta kila wiki. Juma anabaki na Tsh 62,500 ya hela ya UWABA.

### **Video ya usalama wa baisikeli**

Baada ya mkutano tulienda kwenye internet café na tuliangalia video ya UWABA ya usalama wa baiskeli ambayo Amar alitengeneza. Wanachama walipenda sana video a lot na inapendeza sana. Tutaiweka kwenye DVDs na kwenye website na tutasambaza kwa stesheni za TV.

### **Mambo mengine**

Idrisi aliomba vipeperushi vya UWABA ili akisafiri kwa ajili ya mashindano ya baiskeli anaweza kuvisambaza.